

Simamia habari zako za afya kwa usalama, katika sehemu moja

Matibabu salama katika dharura

Katika dharura ya matibabu, wahudumu wako wa afya wanaweza kuona haraka mawasiliano yako ya dharura na miili yako yote, madawa na chanjo, ikiwa imeongezwa. Hii husaidia watoa huduma wako wa afya kukupa matibabu na ustawi kwa salama.

Ipo usiku na mchana

Maelezo yako ya afya yanapatikana wakati wowote unahitaji kwa usalama katika sehemu moja popote ulipo.

Habari sahihi

Katika Rekodi ya Afya Yangu (My Health Record), unaweza kuona na kuangalia maelezo yako ya afya. Hii husaidia wahudumu wako wa afya kukupa tiba sahihi.

Inakusaidia kukumbuka

Rekodi ya Afya yangu inakusaidia kukumbuka maelezo yako ya matibabu. Hii husaidia wakati unapoona wahudumu mbalimbali wa afya.

Haraka na urahisi

Unapowaona wahudumu wa afya katika maeneo tofauti, Rekodi ya Afya Yangu ina ufasaha wa kurahisisha huduma za afya kwako na wahudumu wa afya na huchukua muda mdogo wa kusubiri matokeo ya vipimo na habari kutumwa kati ya wahudumu wa afya.



Swahili

Endelea kufuatilia, sehemu yoyote ulipo

Rekodi yako ya Afya Yangu inakusaidia kuweka ufuatiliaji wa vipimo vyako, matibabu yako, madawa na chanjo, hata wakati unasafiri.

Udhhibiti wa anayeweza kuona maelezo yako ya afya

Katika Rekodi ya Afya Yangu, unaweza kuona orodha ya nani ameangalia rekodi yako na wakati gani. Ikiwa unataka usiri wa ziada, unaweza kuweka nambari ya siri ili kuzuia watu ambao wanaweza kuona rekodi yako au nyaraka za kibinafsi ndani yake, na unaweza kufuta nyaraka wakati wowote.



Ni kinyume na sheria kwa mtu kutazama rekodi yako, isipokuwa ni kwa ajili ya kukupa huduma za afya. Sheria imeweka adhabu kali kwa mwenye atapatikana.

Ikiwa unafikiri mtu ametazama kwa makusudi rekodi yako wakati hawapaswi kufanya hivo, wasiliana na sisi kupitia nambari hii 1800 723 471.



Jinsi ya kuangalia Rekodi yako ya Afya kwa mara ya kwanza

Tumia mtandao myGov kuangalia Rekodi Yako ya Afya. myGov ni njia salama ya kutumia huduma nyingi za Serikali ya Australia kwenye mtandao.

1. Nenda kwenye my.gov.au ili kuweka sahihi kwenye akaunti ya myGov.
2. Chagua 'Services "Huduma'.
3. Chagua 'Link another service "Unganisho na huduma zingine'.
4. Chagua 'My Health Record "Rekodi ya Afya Yangu'.
5. Hakikisha utambulisho wako.

Kama huna akaunti ya myGov, unaweza kufungua akaunti kwenye my.gov.au.

Kuongeza kwenye rekodi yako

Unapoangalia rekodi yako ya kwanza, huenda hakuna taarifa nyingi ndani yake, kama vile Rekodi zako za zamani za matibabu na matokeo ya vipimo. Wewe au mhudumu wako wa afya anaweza kuanza kuongeza habari mpya kwenye rekodi zako za Afya wakati wowote.

Kuongeza habari na matokeo kwenye Rekodi yako ya Afya Yangu, ingia kwenye Rekodi za Afya Yangu kupitia my.gov.au



Weka matokeo mpya kwenye faili yako

Tazama na pia simamia habari zako binafsi.



Ongeza nambari za mawasiliano ya dharura

Weka nambari ya mtu ambaye ungependa apigiwe wakati wa dharura.



Weka jinsi ya kupata taarifa za kila mara

Chagua ikiwa ungependa kujulishwa wakati wowote ambaye mtu anaangalia rekodi yako.



Kuweka habari za Medicare

Chagua maelezo ya Medicare yanayoongezwa kwenye rekodi yako. Hii inaweza kujumuisha madai ya huduma za matibabu kama ziara za daktari, vipimo na madawa, maamuzi yako ya mchango wa viungo, na chanjo zako.



Weka muhtasari wa habari binafsi

Ongeza maelezo yako mwenyewe kuhusu dawa zako na miili.

Uliza mhudumu anayehusika akuwekee muhtasari wa vikao na matokeo vyako kwenye Rekodi ya Afya Yangu

Fanya utafiti zaidi kuhusu Rekodi ya Afya Yangu kwenye:

MyHealthRecord.gov.au

Nambari ya usaidizi (Help line) **1800 723 471**

Kwa msaada katika kiswahili, piga Huduma ya Ukarimani na Utafsiri Taifa (TIS National) kwa **131 450**



Australian Government
Australian Digital Health Agency